*Kioo cha Lugha, Juz. 23(2), 353-368*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i2.10

# Ushiriki wa Watoto katika Vita dhidi ya Utumwa na Harakati za Kupinga Ukoloni nchini Tanzania: Uchunguzi wa Kazi Teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

*Leonard H. Bakize*[1]

## Ikisiri

Makala hii inachunguza ushiriki wa watoto katika vita dhidi ya utumwa na ujio wa wakoloni nchini Tanzania kupitia uchambuzi wa kazi teule za fasihi ya watoto na mwitiko wa wasomaji wa matini hizo. Tofauti na mtazamo wa kijamii unaowaona watoto kama kundi lisilo na sauti katika masuala mazito ya kihistoria, makala hii inathibitisha kwamba watoto walihusika moja kwa moja katika matukio hayo, ama kama wahanga na washiriki au kama wahifadhi wa kumbukumbu za kijamii. Makala hii imetumia mbinu mbili kuu: usomaji makini wa matini na majadiliano ya vikundi vya watoto wa shule za msingi (darasa la 5, 6 na 7) katika maeneo ya Dar es Salaam, Bagamoyo, na Morogoro Mjini. Uchambuzi umeongozwa na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa. Nadharia ya kwanza imetumika kueleza namna watoto wanavyotengeneza maana wanaposoma matini za kihistoria, huku ya pili ikifafanua jinsi fasihi inavyounda hisia za utaifa, umoja, na utambulisho wa pamoja. Makala inaonesha kuwa fasihi ya watoto, hasa bunilizi za kihistoria, si chombo cha burudani tu bali pia ni nyenzo ya kijamii na kielimu inayowezesha watoto kushiriki katika ujenzi wa historia, kukuza fikra za ukombozi na kuimarisha utambulisho wa kitaifa. Kupitia usomaji wa matini na mijadala ya vikundi, watoto walionesha uwezo wa kufasiri upya masimulizi ya kihistoria kwa kuhusisha maadili ya utu, haki na usawa, wakijitokeza pia kama sehemu ya watengeneza historia. Kwa kutumia mitazamo ya nadharia hizi mbili, makala inathibitisha kuwa sauti za watoto zina mchango muhimu katika ujenzi wa kumbukumbu na uelewa wa pamoja wa jamii, hivyo, zinapaswa kupewa nafasi stahiki katika tafiti za kifasihi na kihistoria kuhusu Tanzania na Afrika kwa ujumla.

## 1.0 Utangulizi

Historia ya Tanzania haiwezi kueleweka kwa ukamilifu bila kutambua mchango wa makundi yote ya kijamii, wanaume, wanawake na watoto, katika matukio makuu yaliyounda taifa. Kwa muda mrefu, historia imeandikwa na kuhadithiwa kupitia mitazamo ya watu wazima, wanasiasa na mashujaa wa vita waliotukuka huku sauti

[1] Mhadhiri, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania
Baruapepe: leobakize@gmail.com

za watoto na wanawake zikipuuzwa au kudidimizwa na kuwekwa mbali na simulizi kuu (Gwassa, 1969; Omari, 1995; Geiger, 1987, 1996, 1997). Hali hii imeendeleza mtazamo finyu kwamba watoto ni watazamaji wa historia badala ya kuwa washiriki hai wa mabadiliko ya kijamii. Katika muktadha wa kitaaluma, upungufu huu katika historiografia umechangia kuifanya historia ionekane kama masimulizi ya uongozi na mamlaka, badala ya simulizi ya maisha ya kila siku ya jamii nzima.

Katika tafakuri za kihistoria, mfano bora wa kuonesha upungufu huu ni namna harakati za ukombozi wa Tanganyika zilivyohadithiwa. Kwa miongo kadhaa baada ya uhuru, simulizi hizo ziliwaweka wanaume kama mhimili wa mapambano na ujenzi wa taifa, huku wanawake na watoto wakisalia katika vivuli vya historia. Geiger (1987, 1996, 1997) ametoa changamoto kubwa kwa mtazamo huu kupitia tafiti zake za kina kuhusu wanawake wa TANU, akionesha kwamba, uhuru wa Tanganyika haukuwa kazi ya wanaume pekee bali ni matokeo ya juhudi za pamoja, hususan wanawake waliokuwa mstari wa mbele katika harakati za kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Kupitia kazi yake ya *TANU Women: Gender and Culture in the Making of Tanganyikan Nationalism (1955–1965)*, Geiger anabainisha kwamba wanawake walijenga taifa kupitia kile alichokiita "*Women's work of nationalism*"— yaani michango isiyoonekana katika harakati za kitaifa kama malezi, elimu ya kiraia na uhamasishaji wa kijamii. Uchambuzi huu wa kifeministi unatoa msingi wa kuelewa kwa nini pia watoto, kama kundi jingine lenye sauti za chini, wanapaswa kuingizwa katika mjadala wa historia ya ukombozi na ujenzi wa taifa.

Watafiti kama Guha (1988) na Spivak (1988) wamehoji vikali udhaifu wa historiografia ya kikoloni na ya kitaifa ambayo imetengeneza "ukimya wa historia" kwa makundi ya chini katika jamii za wanawake, wafanyakazi, wakulima na watoto. Guha (1988) anasema kuwa historia rasmi imeandikwa kwa sauti za walio juu, huku waliokuwa wakiteseka au waliopinga mfumo wa kikoloni wakibaki hawasikiki. Katika makala yake ya *Can the Subaltern Speak?* Spivak (1988) anasisitiza kwamba makundi haya ya "wasiosikika" yanaweza kuzungumza, lakini mfumo wa maarifa na lugha unazizuia sauti zao kufikishwa. Mtazamo huu unatoa msingi wa kinadharia kwa makala hii, ambayo inataka kuonesha kwamba watoto kama kundi la kijamii lenye nafasi ndogo katika mamlaka ya kisiasa na kielimu wanaweza "kuzungumza" kupitia fasihi na tafsiri za kihistoria.

Mjadala wa ukombozi wa watumwa na harakati za kupinga utumwa katika Afrika Mashariki umechunguzwa kwa upana, lakini kwa kiasi kikubwa umeelekeza macho kwa viongozi, mashujaa na taasisi za kidini au kiserikali. Tafiti za kihistoria kama za Gwassa (1969) na Omari (1995) zimebainisha kwamba upinzani wa Waafrika dhidi ya wakoloni haukuwa wa kihisia pekee, bali ulipangwa kwa busara na mikakati ya ndani. Hata hivyo, tafiti hizo hazikupenyeza katika maisha ya watoto waliokuwa sehemu ya jamii hizo za wapinzani. Wengi walitumikishwa kama wapasha habari, wapelekaji wa barua, wahudumu wa jeshi au hata wahanga wa moja

kwa moja wa utumwa. Uelewa huu umechukua muda mrefu kujengeka katika utafiti wa Afrika Mashariki.

Alpers (1983) katika sura yake "The Story of Swema: Female Vulnerability in Nineteenth-Century East Africa", anaeleza simulizi ya Binti Swema, msichana wa Kiafrika aliyechukuliwa utumwani, akapata uhuru, na baadaye akaishi maisha ya kiimani. Simulizi hii, licha ya kuwa moja tu kati ya chache, inatoa mwanga wa kipekee juu ya jinsi watoto na wasichana walivyokuwa wahanga na pia wahifadhi wa kumbukumbu za mateso ya utumwa. Naye Kollman (2005), kupitia sehemu ya kitabu chake *The Evangelization of Slaves and Catholic Origins in Eastern Africa*, anachambua upya simulizi la Swema akilitazama si tu kama historia bali kama kipengele cha tafsiri ya kiimani na kijamii. Uchambuzi wa tafiti hizi mbili unaonesha kuwa simulizi za watoto na wanawake walioathiriwa na utumwa si za mateso pekee, bali ni vielelezo vya ujasiri, imani na matumaini, dhima ambazo ndizo kiini cha fasihi ya watoto hasa ile inayobeba historia ya jamii.

Kwa kuunganisha hoja hizi, makala hii inaingia katika mjadala mpana wa utafiti unaojaribu kuandika upya historia kwa mtazamo wa "historia kutoka chini" kama anavyoeleza Nyachoga na Liebst (2024) kuwa, wapo Waafrika waliopata uhuru kutoka utumwani na wakawa vinara wa ukombozi na upatanisho wa kijamii. Hawa ni "wakomesha utumwa" wa Kiafrika waliotoka katika jamii zenye historia ya utumwa na baadaye wakawa walimu wa maadili, viongozi wa kijamii au waenezaji wa amani. Mtazamo huu unapanua uelewa wa historia ya ukombozi kwa kuonesha kwamba sauti za chini, zikiwamo za watoto, hazipaswi kupuuzwa katika ujenzi wa kumbukumbu za kitaifa.

Msingi wa hoja hii unaungwa mkono pia na kazi za Msacky (2024) na Solomon (2024) ambazo zinachunguza urithi wa utumwa katika Bagamoyo na Ujiji. Msacky anaeleza kwamba kumbukumbu za utumwa zimeendelea kuwa sehemu ya utambulisho wa kijamii na historia ya watu wa pwani, huku Solomon akionesha jinsi simulizi za vizazi vya baada ya utumwa zinavyoendelea kujenga uelewa wa uhuru na utu. Kwa mtazamo huu, fasihi ya watoto inakuwa chombo cha kiutamaduni kinachoendeleza urithi huo wa kihistoria kwa lugha nyepesi lakini zenye maana kubwa kwa kizazi kipya.

Kwa mujibu wa *Muhtasari wa Somo la Historia kwa Shule za Msingi* (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2006), madhumuni ya kufundisha historia ni kuwawezesha wanafunzi "kuelewa chimbuko la jamii yao na matukio yaliyosababisha mabadiliko katika jamii za Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla." Somo hili linakusudia pia kujenga uwezo wa kuchambua na kutathmini utamaduni, kukuza umoja wa kitaifa na ushirikiano, pamoja na kukuza stadi za kufikiri kiyakinifu na kujitegemea kifikra na kimatendo. Maelekezo haya yanaashiria kwamba watoto wanapaswa kuwa washiriki hai wa historia, si tu wapokeaji wa maarifa bali wahifadhi na wabunifu wa kumbukumbu za kitaifa pia. Kadhalika, *Muhtasari wa Somo la Uraia kwa Shule za Msingi* (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2006), unasisitiza umuhimu wa kuwajenga wanafunzi kuwa raia wema,

wenye kuelewa mfumo wa siasa, haki na wajibu wao katika kujenga taifa. Uhusiano huu kati ya historia na uraia unaimarisha dhana kuwa mtoto ni sehemu ya mchakato wa ujenzi wa taifa; si kiumbe asiye na sauti.

Kwa mtazamo wa kijamii, historia ya Tanzania inaonesha kuwa watoto walihusishwa katika harakati za ukombozi kwa njia nyingi. Wengine walitumika kama wapasha habari katika vita, walisaidia katika kazi za ngome au walibeba vifaa vya wapiganaji. Wengine, hasa katika maeneo ya pwani kama Bagamoyo, walishuhudia kwa macho yao biashara ya utumwa, jambo lililowaathiri kisaikolojia na kuwa chachu ya uzalendo wa baadaye. Kuwapo kwa watoto katika matukio haya kunathibitisha kwamba walikuwa sehemu ya jamii inayojifunza na kushiriki katika mabadiliko ya kihistoria. Kwa mujibu wa Gwassa (1969), upinzani wa Waafrika dhidi ya wakoloni haukuwa wa ghafla bali ulijengwa kwa busara na mpangilio wa ndani; hivyo, ni wazi kuwa watoto waliingizwa katika mfumo wa kijamii uliotengeneza vizazi vya wazalendo.

Kwa upande mwingine, Omari (1995) anaeleza kuwa mafanikio makubwa ya Tanzania katika kudumisha umoja wa kitaifa yamejengwa katika msingi wa falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea iliyoasisiwa na Mwalimu Julius K. Nyerere. Falsafa hii ilisisitiza umoja, usawa na utu wa binadamu, maadili ambayo yalijengwa tangu utotoni kupitia elimu, michezo na simulizi za kifasihi. Methali ya Kiswahili isemayo, 'samaki mkunje angali mbichi' inabeba maana ya kwamba malezi ya kitaifa na kihistoria huanza utotoni. Hivyo, fasihi ya watoto ni sehemu ya mchakato wa kitaifa wa kujenga maadili ya uzalendo, utu, na umoja. Vivyo hivyo, methali nyingine isemayo, 'mtoto wa nyoka ni nyoka' inaashiria kwamba watoto ni warithi wa historia ya vizazi vilivyotangulia — warithi wa mapambano, matumaini na uthubutu.

Fasihi ya watoto, kama wanavyoeleza Lyimo (2014), Ngugi (2016), na Bakize na wenzake (2017), ni chombo cha kijamii na kielimu kinachobeba historia, maadili na fikra za ukombozi. Kupitia usomaji wa kazi kama *Wimbo wa Sokomoko* (1990) iliyoandikwa na Amandina Lihamba na riwaya tatu za *Ngoma ya Mianzi* (1991), *Ngome ya Mianzi* (1991) na *Moto wa Mianzi* (1996) zilizoandikwa na Mugyabuzo Mlinzi Mulokozi, watoto hujifunza kuhusu historia ya taifa lao, wajibu wa kulinda utu wa binadamu, na umuhimu wa ushirikiano katika mapambano ya kijamii. Katika kazi hizi, watoto wanajitokeza si kama wahanga wa utumwa au ukoloni tu, bali kama wahusika pia wenye nguvu ya kiakili, kimaadili na kivitendo ambao wanaweza kupanga, kuamua na kutenda kwa manufaa ya jamii yao.

Kwa mtazamo wa kifasihi, nadharia mbili zimeongoza utafiti huu: Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji (Rosenblatt, 1978; Fish, 1980) na Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa (Anderson, 1983). Nadharia ya kwanza inasisitiza kuwa maana ya matini haipo ndani ya maandiko pekee bali hutengenezwa na msomaji katika mchakato wa usomaji. Hivyo, watoto kama wasomaji wana uwezo wa kuunda maana mpya za kihistoria wanaposoma matini zenye dhamira ya utumwa na ukombozi. Nadharia ya pili inaeleza kuwa jamii na utaifa ni matokeo ya simulizi za

pamoja zinazobuniwa na wanajamii. Hivyo, kupitia fasihi, watoto wanajengewa hisia za jumuiya, utaifa na urithi wa pamoja.

Kwa misingi hii, makala hii inasisitiza kwamba historia, uraia na fasihi ya watoto vinafungamana katika kuendeleza maadili ya umoja, utu, na uhuru. Watoto hawakuwa watazamaji bali walikuwa washiriki wa uhai wa jamii, waandishi wa kimya wa historia. Methali ya Kiswahili, 'usione vyaelea, vimeundwa', inaikumbusha jamii kwamba umoja, amani na maendeleo ya taifa la Tanzania vimejengwa juu ya juhudi za pamoja, ikiwamo juhudi za watoto. Hivyo, fasihi ya watoto inakuwa kiunganishi kati ya historia na vizazi, daraja kati ya ukombozi wa jana na matumaini ya kesho.

## 2.0 Mapitio ya Machapisho na Pengo la Utafiti Lililoshughulikiwa

Fasihi ya kihistoria ya watoto nchini Tanzania imeibuka kama uwanja muhimu wa kuwasilisha historia, maadili na fikra za ukombozi wa kijamii. Hata hivyo, katika tafiti nyingi za kihistoria na kifasihi, nafasi ya watoto imekuwa ikitazamwa kama ya upokeaji tu wa urithi wa kihistoria, badala ya ushiriki hai katika mabadiliko ya kijamii. Tafiti za awali za kihistoria (Gwassa, 1969; Omari, 1995) ziliangazia zaidi mashujaa wakuu na viongozi waliopigania ukombozi, huku wakipuuza mchango wa watoto kama wahusika wenye uwezo wa kufikiri, kushiriki na kuelezea maana ya uhuru kwa mitazamo yao.

Katika miaka ya hivi karibuni, tafiti mpya zimeanza kutafakari upya uelewa wa ukombozi katika historia ya Afrika Mashariki, zikitoa nafasi kwa sauti zilizokuwa zimesahaulika. Nyachoga na Liebst (2024) wamesisitiza kwamba Waafrika wenyewe walikuwa nguzo kuu ya ukomeshaji wa utumwa, si waathirika tu. Msacky (2024) na Solomon (2024) nao wameonesha jinsi kumbukumbu za utumwa Bagamoyo na Ujiji zilivyoendelea kuunda urithi wa kijamii na uelewa wa historia kwa vizazi vipya. Tafiti hizi zinatoa msukumo kwa makala hii kwa kuwa zinathibitisha kwamba ukombozi wa Mwafrika haukuwa kazi ya wageni pekee bali matokeo ya mwamko wa ndani unaotokana na uzoefu wa kijamii na kiutamaduni.

Vivyo hivyo, tafiti za kifasihi (Omari, 2009; Lyimo, 2014; Ngugi, 2016; Bakize na wenzake, 2017; Mosha, 2017; Mahenge, 2020, kwa kutaja chache) zimechambua kwa kina maudhui ya kijamii katika maandiko ya watoto, lakini hazijatoa tafakuri ya kutosha kuhusu namna watoto, kama wasomaji na wahusika, wanavyoshiriki katika kuunda maana za kihistoria. Pengo hili la kitaaluma linaibua maswali muhimu: Je, watoto wana nafasi gani katika historia ya mapambano dhidi ya utumwa na ukoloni, na fasihi ya watoto inaweza kutumika vipi kama nyenzo ya kuwajenga watoto wa Kitanzania kuwa sehemu ya kumbukumbu na utambulisho wa taifa lao?

Katika muktadha huo, fasihi ya watoto inajitokeza kama chombo cha kubadilisha fikra na mitazamo kuhusu historia ya utumwa. Kazi za Lihamba (*Wimbo wa Sokomoko*, 1990) na Mulokozi (*Ngoma ya Mianzi*, 1991; *Ngome ya Mianzi*, 1991; *Moto wa Mianzi*, 1996) zinaibua simulizi ambapo watoto wanageuzwa kuwa

wahusika wakuu wa mapambano ya uhuru. Katika hadithi hizi, watoto kama Mbumi, Chulu, Mugoha na Nyawelu wanapewa nafasi ya kutenda na kufikiri, wakiongozwa na misingi ya utu, ujasiri na mapambano ya kijamii. Wanaibuka kama watetezi wa jamii zao, wakiwakilisha kizazi kipya kinachoendeleza mapambano ya wazee kwa lugha ya ubunifu wa kifasihi. Kwa namna hii, fasihi inachukua nafasi ya kufundisha historia kwa njia ya mwitiko wa kihisia na kiakili, ambapo watoto wanajifunza kuhusisha mapambano ya kihistoria na uhalisia wa maisha yao ya sasa.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji (Rosenblatt, 1978; Fish, 1980), maana ya matini hutengenezwa katika mwingiliano kati ya msomaji na maandiko. Hivyo, watoto wanaposhiriki kusoma hadithi zenye dhamira ya utumwa na ukombozi, wanakuwa washiriki wa ujenzi wa maana mpya za historia. Hali hii inaungwa mkono na Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa (Anderson, 1983) ambayo inabainisha kuwa hisia za utaifa na umoja wa kijamii hujengwa kupitia masimulizi yanayoshirikisha hisia na kumbukumbu za pamoja. Kwa kutumia nadharia hizi, makala hii inaeleza jinsi watoto, kupitia usomaji wa kazi za kifasihi, wanavyounganishwa na historia ya mapambano ya kitaifa na kijamii.

Kwa upande wa elimu, mfumo wa ufundishaji historia nchini Tanzania bado una changamoto ya kuendeleza mtazamo wa kihistoria unaojumuisha watoto kama wahusika hai wa historia. Kama anavyobainisha Nyanto (2022) katika makala yake "Decolonizing Curriculum: Slavery, Empire, and History Teaching in Tanzania, 1961-2022," mada ya utumwa imeendelea kufundishwa kama sehemu ndogo ndani ya historia ya ukoloni, bila kuonesha mchango wa Waafrika, hususan watoto, katika harakati za ukombozi. Hivyo, makala hii inajitokeza kama mchango wa kipekee katika mjadala wa kitaaluma kwa kuunganisha fasihi, historia na elimu ya watoto ili kuonesha kwamba ukombozi si tukio la kihistoria pekee bali ni mchakato endelevu wa kiutamaduni, kiakili na kijamii.

Kwa jumla, makala hii inajenga hoja kwamba fasihi ya watoto si chombo cha kuburudisha tu, bali ni jukwaa la kitaaluma pia linalowawezesha watoto kutafakari historia ya utumwa kama sehemu ya utambulisho wao. Kwa njia hii, watoto wanajifunza si tu kuhusu wanyonyaji wa kale bali pia kuhusu wajibu wao katika kulinda utu, haki na uhuru wa jamii yao leo. Hivyo, fasihi inakuwa si tu nyenzo ya kielimu bali pia silaha ya kiutamaduni inayofundisha ukombozi kwa vizazi vipya.

## 3.0 Methodolojia

Makala hii imetokana na utafiti wa kitaamuli. Utafiti wa kitaamuli umetumika kwa kuwa unamwezesha mtafiti kufanya uchunguzi wa kina wa kisayansi kwa njia ya tafakuri na kuchanganua mambo maalumu kwa lengo la kupata maarifa mapya au kuongeza ufahamu (Ponera, 2019). Makala ilitumia data zilizopatikana kwa kutumia mbinu kuu tatu. Kwanza, makala hii ilitumia mbinu ya usomaji makini wa matini teule zinazohusu historia ya utumwa na ukoloni, hususan *Wimbo wa Sokomoko* (Lihamba, 1990) na riwaya za Mulokozi za *Ngoma ya Mianzi* (1991), *Ngome ya*

*Mianzi* (1991) na *Moto wa Mianzi* (1996). Uteuzi wa matini hizi ulizingatia kigezo kikuu cha kusheheni matukio ya kihistoria ambayo pia yamesimuliwa katika kazi nyingine zisizo za kifasihi. Uchambuzi huu ulisaidia kubaini namna waandishi wanavyowasilisha historia na kuibua sauti za watoto katika matini za kifasihi.

Pili, zilikusanywa data za uwandani kupitia mijadala ya watoto wanafunzi katika shule tano (5) za Tanzania, ambazo ni Shule ya Msingi Mkundi (Morogoro),[2] Shule ya Msingi SUA (Morogoro),[3] Shule ya Msingi Kizuiani (Bagamoyo),[4] Shule ya Msingi Mwambao (Bagamoyo),[5] na Shule ya Msingi Uhuru Wasichana (Dar es Salaam).[6] Shule hizi ziliteuliwa kutokana na taarifa za awali alizokuwa nazo mtafiti kwamba katika maktaba za watoto za shule hizo, zilizokuwa chini ya Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania, kulikuwa na vitabu teule vya kihistoria ambavyo vimechambuliwa katika makala hii. Watoto 6-8 (wavulana na wasichana kwa usawa) wa darasa la 5-7[7] kwa kila shule waliosoma vitabu teule waliteuliwa kushiriki katika mjadala wa vikundi. Upatikanaji wa watoto hawa ulitokana na taarifa za msimamizi wa maktaba za watoto kwa kila shule. Wasimamizi wa maktaba za watoto katika shule husika waliteua watoto waliohusika katika utafiti kwa kuwa wao walikuwa wanafahamu uwezo wa watoto wasomaji. Vitabu teule vilivyohusika katika mjadala ni vile vinavyohusiana na historia ya utumwa na ujio wa wakoloni. Data za aina hii zilikusanywa kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2018 mpaka mwaka 2020. Mijadala hiyo ya wanafunzi ililenga kufahamu namna watoto wanavyofasili matukio ya kihistoria, maadili ya kijamii na uelewa wa utu kupitia simulizi za kifasihi, hasa riwaya za kihistoria.

Tatu, utafiti umezingatia upitiaji wa machapisho ya kitaaluma kutoka ndani na nje ya Tanzania ili kuimarisha hoja na kuweka matokeo ya utafiti huu katika muktadha mpana wa kitaaluma. Uchanganuzi wa data umefuata kanuni za Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Jumuiya Zilizobuniwa, ambazo zimewezesha kutafsiri mitazamo ya watoto na kazi za fasihi kama nyenzo za ujenzi wa kumbukumbu na utambulisho wa kihistoria.

## 4.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala hii imeongozwa na mawazo ya nadharia mbili kuu: Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa. Nadharia hizi zimetumika kwa pamoja ili kujenga uelewa wa kina kuhusu namna watoto wanavyoshiriki katika kutengeneza maana za kihistoria na kijamii kupitia usomaji wa fasihi na uzoefu wa kijamii unaohusiana na historia ya utumwa na ukoloni.

---

[2] Mjadala ulifanyika tarehe 17.07.2018.
[3] Mjadala ulifanyika tarehe 18.07.2018.
[4] Mjadala ulifanyika tarehe 23.08.2019.
[5] Mjadala ulifanyika tarehe 24.07.2018.
[6] Mjadala ulifanyika tarehe 30.06.2020.
[7] Watoto wa madarasa haya ndio waliokuwa na uwezo wa kusoma vitabu husika na kuvielewa kutokana na umri na urazini wao.

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, iliyoasisiwa na Louise Rosenblatt (1978) na baadaye kuendelezwa na Stanley Fish (1980), inasisitiza kuwa maana ya matini haipo ndani ya maandiko pekee, bali inatengenezwa na msomaji pia katika mchakato wa kusoma. Rosenblatt (1978) alieleza kwamba uhusiano kati ya msomaji na maandiko ni wa kivitendo, ambapo kila msomaji huchangia kuunda maana kulingana na uzoefu, hisia na muktadha wake wa kijamii. Fish (1980) aliipanua hoja hii kwa kubainisha kuwa tafsiri za wasomaji hutegemea mitazamo ya kijamii na kikundi cha kiutamaduni wanachotoka. Aidha, hoja nyingine ya msingi ni kwamba usomaji wa matini, hasa za kifasihi, huwa na maana nyingi kutokana na hali ya wasomaji na huwabadilisha wasomaji kifikra na kimtazamo (Wamitila, 2002; Njogu, 2007).

Kwa upande mwingine, Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa iliyoasisiwa na Benedict Anderson (1983), inatoa msingi wa kuelewa jinsi jamii zinavyojibuni kupitia simulizi, lugha, na kumbukumbu za pamoja. Anderson anaeleza kwamba taifa ni "jumuiya iliyobuniwa" kwa sababu wanajamii wake, ingawa hawajuani wote na kuonana ana kwa ana, wanashirikiana katika hisia ya umoja na utambulisho unaotokana na historia, lugha na utamaduni. Nadharia hii inasaidia kuelewa jinsi fasihi ya watoto inavyotumika kujenga kumbukumbu na hisia za utaifa miongoni mwa watoto. Kupitia hadithi na mijadala ya kihistoria, watoto wanajiona kama sehemu ya taifa lenye urithi wa pamoja wa mapambano, utu na uhuru.

Kwa hiyo, muunganiko wa nadharia hizi mbili unarahisisha uchambuzi wa namna watoto wanavyoshiriki katika ujenzi wa historia na utambulisho wa kitaifa. Mwitiko wa Msomaji unatoa jukwaa la kuelewa tafsiri binafsi za watoto kuhusu historia, huku Jumuiya Zilizobuniwa ikifafanua namna tafsiri hizo zinavyochangia kuunda kumbukumbu na umoja wa kitaifa. Hivyo, nadharia hizi zimeiwezesha makala hii kuonesha kuwa watoto hawako tu kama wasomaji wa historia bali nao ni wahusika wanaobuni, kuelewa na kuendeleza simulizi za taifa lao kupitia fasihi na elimu ya kihistoria.

## 5.0 Uchambuzi wa Data

Sehemu hii inawasilisha uchambuzi wa kina wa data zilizokusanywa kupitia mbinu mbili kuu: usomaji makini wa matini teule za fasihi ya watoto na mijadala ya vikundi iliyofanyika katika shule za msingi za Dar es Salaam, Bagamoyo na Morogoro mjini. Vipengele hivi viwili vinaungana ili kutoa taswira pana ya namna watoto wanavyojengwa, wanavyowasilishwa, na wanavyofasili historia ya utumwa na ukoloni katika muktadha wa Tanzania. Kwa kutumia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji (Rosenblatt, 1978; Fish, 1980), uchambuzi unazingatia namna watoto kama wasomaji wanavyotengeneza maana kupitia hisia, uzoefu na utambulisho wao wa kijamii. Vivyo hivyo, kupitia Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa (Anderson, 1983), matini na maelezo ya watoto yanachunguzwa kama vyanzo vya ukusanyaji wa kumbukumbu za taifa na ujenzi wa utambulisho wa pamoja.

Uchambuzi pia unategemea misingi ya kihistoria iliyoainishwa na wanahistoria kama Gwassa (1969), Alpers (1983), Msacky (2024) na Solomon (2024), ambayo inaonesha namna watu kutoka makundi yaliyosahaulika, wakiwamo wanawake, vijana na watumwa waliokombolewa, walivyohusika katika upinzani dhidi ya utumwa na ukoloni. Hivyo, data hii inaleta mwanga mpya kwa kuonesha kuwa watoto, kama wahusika wa fasihi na wasomaji, ni sehemu muhimu ya urithi wa mapambano haya.

Kwa ujumla, uchambuzi huu unaonesha jinsi simulizi za fasihi ya watoto zinavyogeuka kuwa darasa hai la historia na uraia, jinsi watoto wanavyofasili upya masimulizi ya kijamii, na namna fasihi inavyotumika kama chombo cha kuendeleza kumbukumbu ya ukombozi na kuimarisha utambulisho wa kitaifa. Sehemu zinazofuata zinajadili kwa kina vipengele hivi kwa kuzingatia uhusiano kati ya fasihi, historia na uzoefu wa watoto wa kisasa.

### 5.1 Watoto kama Wahusika Washiriki wa Historia ya Utumwa na Ukoloni

Matini teule, yaani kazi ya Lihamba (*Wimbo wa Sokomoko*, 1990) na Mulokozi (*Ngoma ya Mianzi*, 1991; *Ngome ya Mianzi*, 1991 na *Moto wa Mianzi*, 1996), zinawaweka watoto katikati ya historia ya kupinga utumwa na ukoloni, na hivyo, kubadili mkondo wa simulizi za "mashujaa watu wazima" kuwa simulizi jumuishi za kizazi chote, hususan watoto. Kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji; maana ya ujasiri, uzalendo na wajibu inaibuliwa katika mwingiliano wa msomaji mdogo na matini; na kupitia Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa, simulizi hizi zinabuni hisia ya taifa inayounganisha vizazi kama inavyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

#### (a) Uzalendo, Umoja na Alama za Mapambano

Katika *Wimbo wa Sokomoko*, wimbo wa utangulizi wa simulizi unaweka "kiapo cha kizazi": Wimbo unasema, "Sisi shujaa kabisa, Sokomoko Sokomoko, watoto wa vita" (uk. 1). Huu ni mwito wa kijumla unaowaleta watoto kama "jeshi dogo" la maadili ya taifa. Aidha, falsafa ya kijamii inasisitizwa: "Uchoyo adui yetu, utumwa hatutaki kwetu, ujangili si mwenzetu" (uk. 3). Kwa Mwitiko wa Msomaji, maneno haya hutafsiriwa na watoto kama mwaliko wa kupinga dhuluma na ubinafsi; kwa Jumuiya Zilizobuniwa, ni alama za "kanuni za taifa" linalojitambua kwa kumbukumbu ya pamoja.

Katika *Ngoma ya Mianzi*, urithishaji wa jukumu la kizazi unatiwa muhuri kwa mkuki: "Watoto walikabidhiwa mkuki mkuu wa mianzi, ishara ya ujumbe wa kivita kwenda kwa Mutwa Mukwava" (uk. 11). Mkuki hapa si chuma tu; bali ni ishara ya kupokezana "enzi ya uwajibikaji." Watoto hawabebi silaha pekee, bali hadhira mpya ya kumbukumbu kwani wanapewa "kazi ya taifa" kama wapasha habari, kuwa wapelelezi na wasimamizi wa siri za jamii (*Ngoma ya Mianzi*, taz. kur. 8, 43 na 44).

**(b) Ushujaa wa Watoto katika Kupambania Taifa**

Ushujaa wa watoto hauchorwi kwa maneno matupu bali unachorwa pia kwa visa, adabu na hatari. Katika *Wimbo wa Sokomoko* tunasoma: "Silaha zetu si haba, tumepewa na wahenga, Bagamoyo, Ujiji, hasa Kw'iloza" (uk. 1). Hapa "silaha" ni urithi wa kizazi: busara, weledi, ujasiri, na falsafa ya kusimama na wanyonge. *Ngoma ya Mianzi* inaweka kiwango cha juu cha uvumilivu na kutunza siri: "Tuko tayari kufa kwa ajili ya wengine… hata tukiteswa hatuko tayari kutoa siri" (kur. 43-44). Hii inaoana na ushahidi wa kihistoria kwamba huenda wapasha habari, wajumbe na vijana waliwahi kutumika katika mapambano ya upinzani dhidi ya utumwa na ukoloni (Gwassa, 1969; Geiger, 1997).

Katika *Ngome ya Mianzi*, historia inafungwa moja kwa moja na jina la mtoto: "Mugoha alipewa jina kutokana na vita… Mugoha maana yake ni mkuki" (uk. 1). Hilo ni jina linalomweka mhusika kama alama ya kizazi kinachofuata, kinachoitwa kuendeleza maadili.

**(c) Uvunjaji wa Mfumodume ili Kulinda Umoja wa Kitaifa**

Ushujaa wa wasichana unachorwa kwa uthabiti. *Wimbo wa Sokomoko* unamjenga Mbumi kama kiongozi wa kike: "Mbumi alikuwa na akili nyingi za ubunifu… alibaki hodari hata pale Chulu alipoanza kukata tamaa" (kur. 9-11). Katika *Ngoma ya Mianzi* tunasoma: "Mbumi hakutaka kukaa kizembezembe… alikuwa mkali, mjanja na jasiri. Wala hakuogopa kifo" (kur. 34-37). Katika *Ngome ya Mianzi*, sauti ya Nyawelu inachochea falsafa: "Mtu anaweza kukishinda kifo?" (uk. 16). Vilevile, katika *Moto wa Mianzi*: "Nyawelu alikuwa mvumilivu na mkomavu; aliweza kustahimili wakati sisi tuliojiita wanaume tukiporomoka kama vifusi" (uk. 27). Mstari huu "unamnyanyua" msichana kama nguzo ya maadili na utendaji. Kihistoria, utafiti wa Geiger (1987, 1996, 1997) umeonesha kwamba simulizi rasmi za ujenzi wa taifa zilipuuza kazi ya wanawake/wasichana. Sasa matini hizi zinarejesha mizani ili kusawazisha kumbukumbu za kihistoria zinazopaswa kuenziwa vizazi na vizaki katika kulinda mshikamano wa kitaifa.

**5.2 Watoto kama Wasomaji Wanaofasili Upya Historia**

Katika kipengele hiki tutaona fasili mbalimbali ambazo wasomaji watoto walizitoa kutokana na welewa wao wa matini teule walizokuwa wamesoma kabla ya mijadala ya vikundi. Katika kila kipengele, uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kama ifuatavyo:

**(a) Uelewa wa Ujasiri na Uzalendo**

Katika mjadala uliofanyika katika Shule ya Msingi Uhuru Wasichana (Dar es Salaam), msichana wa Darasa la 5A: alisisitiza, "Nimejifunza kuwa jasiri na mvumilivu… (na) kutunza siri za nchi kama walivyofanya akina Mugoha na Nyawelu… Ninatamani kuwa kama vijana hawa Mbumi na Chulu… wanaojitoa

mhanga kwa ajili ya jamii yao.” Hii ni fasili ya moja kwa moja ya mistari ya Mulokozi kuhusu kutotoa siri (taz. *Ngoma ya Mianzi*, kur. 43-44) na ya Lihamba kuhusu uzalendo na umoja (*Wimbo wa Sokomoko*, kur. 1-3). Watoto “wanaunda maana” kwamba kujitahidi shuleni, kuaminika na kushirikiana ni mwendelezo wa mapambano ya kihistoria.

Katika Shule ya Msingi SUA (Morogoro), mvulana wa Darasa la VI alisema wakati wa mjadala: “Nimewapenda Mbumi na Chulu kwa sababu walikuwa na bidii na walipendana mno… Hawakukata tamaa kwa kila jambo.” Kufasili matini huku kunaunganisha ushujaa na unyenyekevu wa uhusiano. Watoto wanatazama mapambano kuwa si vita tu, bali “malezi ya maadili ya pamoja.”

Katika mjadala wa Shule ya Msingi Mwambao (Bagamoyo), mvulana wa Darasa la VII anasema: “Nimejifunza jinsi walivyoshikamana kuwakomesha wakoloni… Siwapendi wakoloni kwa sababu waliwatesa watu wetu…” Kihisia, watoto wa Bagamoyo wanahusisha eneo lao la kumbukumbu na simulizi: masoko ya watumwa (taz. *Wimbo wa Sokomoko*, uk. 22) na ushahidi wa kihistoria wa Bagamoyo (Msacky, 2024; Magumba, 2025). Huu ni mwingiliano wa mahali, historia na msomaji. Haya yote yanakuwa muhimu kwa mtoto anayekuzwa ili kulinda taifa lake.

**(b) Chuki dhidi ya Dhuluma na Usaliti katika Jamii**

Katika mjadala wa Shule ya Msingi Mwambao (Bagamoyo), msichana wa Darasa la VII aliyesoma riwaya ya *Moto wa Mianzi*, alichangia kwa kusema: “Nimependa sana ushirikiano uliokuwepo kwa watoto … Nimemchukia sana Kafugwa kwa sababu alikuwa Mwafrika msaliti…” Kauli hii inabeba kanuni: usitafune taifa lako. Chuki dhidi ya kijana huyu ilitokana na usaliti wa jamii yake (kur. 98-99) ambapo Nyawelu anatimiza adhabu ya msaliti Kafugwa kwa kumchoma sindano ya sumu kimyakimya bila mtu kujua. Pia, dawa ya moyo wa usaliti inarudiwa kwenye *Ngome ya Mianzi* (kur. 26, 29 na 33) ambapo busara na uaminifu vinatajwa kama silaha za jamii iliyoshikamana.

Katika mjadala wa Shule ya Msingi Kizuiani (Bagamoyo), mvulana wa Darasa la VII naye alikiri kwa kusema: “Vitabu hivi vimenifanya nijione kuwa na mimi ninaweza kuwa jasiri, mzalendo, mwenye kuupenda umoja…” Hapa, mwanafunzi anajengwa kisaikolojia kwa kujiona mhusika wa historia. Huu ndio moyo wa Mwitiko wa Msomaji kwa msomaji “kuvaa kiatu” cha mhusika na kukigeuza kuwa chake.

Aidha, wakati wa mjadala katika Shule ya Msingi Kizuiani (Bagamoyo), msichana wa Darasa la V alikazia kwa kusema: “Nimejifunza kupenda nchi yangu na kujitoa mhanga; kutokata tamaa katika kupambania jamii yangu.” Hii “fasili ya maadili” inayochipuka moja kwa moja kutoka *Wimbo wa Sokomoko* (uk. 3) na *Ngoma ya Mianzi* (kur. 43-44). Hizi ni silaha muhimu ambazo watoto wanarithi kwa ajili ya kulinda jamii na taifa lao.

**(c) Tofauti za Kijinsia na Kuibuka kwa Sauti ya Msichana**

Mijadala mingi ilionesha furaha ya wasichana kuona wahusika wa kike wakiwa mstari wa mbele: Mbumi na Nyawelu. Hoja ya "mila" kwamba msichana hashiki mkuki katika *Ngoma ya Mianzi* (kur. 12 na 15) inavunjwa na matendo ya wasichana hawa (kur. 38-42; 58; 61 na63). Watoto wa leo wanaipa maana nafasi ya wahusika wa kike katika kazi hizo kama ushahidi wa uhalali wa uongozi wa kike, sauti ambayo kihistoria Geiger (1996, 1997) aliionesha kuwa ilipuuzwa katika simulizi za ujenzi wa taifa.

**(d) Fasihi ya Kihistoria kama Darasa Hai la Historia na Uraia**

Kauli za watoto katika mijadala zilionesha kwamba vitabu walivyosoma viliwasaidia sana kuelewa historia kwa urahisi. Hii inathibitisha kwamba fasihi – hasa bunilizi za kihistoria, inatimiza kwa vitendo nia ya Muhtasari wa Historia wa Shule za Msingi (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2006) ya "kujenga umoja wa kitaifa, utambuzi na tafakuri." Watoto wanaposoma kifasihi kuhusu Bagamoyo, Uhehe, Lugalo na Kalenga, wanapata hisia za kushiriki katika matukio (taz. *Moto wa Mianzi*, kur. iv–vii; 8; 90), kisha wanayageuza mambo waliyojifunza kuwa tunu zao leo: maadili, uzalendo na umoja.

Malengo ya Muhtasari wa Historia wa Shule za Msingi (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2006) hasa, "kuelewa chimbuko la jamii yao… kujenga umoja na stadi za kufikiri kiyakinifu," yanatimia kupitia hadithi hizi za kihistoria. Watoto wanahusisha Bagamoyo na Ujiji kama vituo vya kumbukumbu (Msacky, 2024; Solomon, 2024). Hivyo, fasihi inakuwa daraja la vizazi na hifadhi ya urithi. Kwa mfano, *Wimbo wa Sokomoko* unagusia sehemu mahususi kama: Bagamoyo: soko la watumwa (uk. 22), misheni (kur. 24-27), kupata dini za kigeni, lugha na teknolojia mpya (kur. 27-28); Usagara na mikataba ya Carl Peters (kur. 17–19); na Kw'iloza kama "eneo lililoshuhudia misafara ya watumwa." Matukio haya, kitaalamu yanakubaliana na utafiti wa Msacky (2024) (urithi wa utumwa Bagamoyo), Magumba (2025) (simulizi mseto) na Solomon (2024) (Ujiji kama kumbukumbu hai za baada ya ukomeshaji wa utumwa).

*Ngoma ya Mianzi* na *Ngome ya Mianzi* zinaiweka Lugalo 1891 na Kalenga 1894 katika muhtasari wa simulizi (*Moto wa Mianzi*, kur. iv, 8 na 64-65). Uhalisia wa kivita — Mkwawa, Von Zelewski (Nyundo)—unakumbukwa kwa mtazamo wa mtoto, na hivyo, historia inapata lugha ya kurithiwa.

**6.0 Mjadala Mfupi**

Matokeo ya uchambuzi wa matini na mijadala ya wanafunzi yanaonesha wazi kuwa fasihi ya watoto imejitokeza kama nyenzo mahususi ya kuwakilisha, kufufua na kuendeleza historia ya mapambano dhidi ya utumwa na ukoloni. Kazi za Lihamba (1990) na Mulokozi (1991a, 1991b, 1996) zinamrejesha mtoto katikati ya historia ya ukombozi, jambo linalovunja na kutikisa historiografia ya jadi iliyowapa watu wazima, viongozi wa vita na wanaume nafasi ya kipekee kama wahusika wakuu wa

mabadiliko ya kihistoria. Uwasilishwaji wa watoto kama Mbumi, Chulu, Mugoha na Nyawelu kama wahusika wanaobeba jukumu la kulinda taifa unathibitisha kuwa simulizi hizi zinaunda mazingira mapya ya ufahamu ambapo mtoto anajiona kama sehemu ya injini ya mabadiliko, si mwangaliaji tu bali mshiriki kamili wa historia.

Kwa kutumia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, tafsiri za watoto wakati wa mijadala zinaonesha kuwa maana ya ujasiri, uzalendo, mwendelezo wa kizazi na kupinga dhuluma haipatikani tu katika matini bali katika mwingiliano baina ya msomaji na simulizi. Wanafunzi kutoka Dar es Salaam, Bagamoyo na Morogoro walionesha kiwango cha juu cha uchakataji wa kihisia na kiakili waliposoma hadithi za mapambano. Walisema, "Nimejifunza kutunza siri za nchi yangu," "Ninataka kuwa jasiri kama Mbumi," au "Nimemchukia Kafugwa kwa sababu ni msaliti." Mwitiko huu unaonesha kuwa watoto walihamishia historia katika ulimwengu wao wa sasa, wakitengeneza maadili mapya yanayolingana na dhana za uraia, utu na uzalendo katika muktadha wa kitaifa.

Kwa upande mwingine, Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa inaonesha kuwa vitabu hivi vinajenga hisia ya "taifa la kufikirika" kupitia alama za pamoja kama wimbo wa Sokomoko, Mkuki wa Mianzi, au mahali kama Bagamoyo, Kw'iloza, Kalenga na Lugalo. Watoto wanapoona nafsi zao katika mashujaa wa fasihi, hasa katika maeneo ambayo kihistoria yalihusishwa na utumwa, wanajijenga kama warithi wa mapambano na kama kinga ya taifa dhidi ya ukoloni mamboleo. Ujumbe wa simulizi, kwamba "watoto wa vita" ni kizazi kinachoendeleza wajibu wa kulipa deni la historia, unaendana na tafiti za kihistoria (k.m. Alpers, 1983; Msacky, 2024; Solomon, 2024; Magumba, 2025) zinazoonesha kuwa vijana, watumwa walioachiliwa na watu wa makundi ya chini waliwahi kuwa kiungo muhimu katika harakati za kiutamaduni na kijamii za baada ya utumwa.

Zaidi ya hayo, uchambuzi umeonesha kuwa simulizi hizi zinachochea mjadala wa kijinsia kwa kuwaongezea wasichana nafasi ya kiushujaa, jambo ambalo linarekebisha historia iliyotawaliwa na mtazamo wa kiume. Wahusika kama Mbumi na Nyawelu wanavunja ukuta wa mfumodume kwa kuongoza vita, kutoa hoja imara za kifalsafa na kuonesha uthabiti uliozidi wa wavulana. Hii inaendana na tafiti za Geiger (1987, 1996, 1997) zinazoonesha kuwa simulizi za kitaifa mara nyingi zilipuuza mchango wa wanawake katika ujenzi wa taifa. Hivyo, fasihi hii inachangia kazi ya kihistoria ya kuzikomboa sauti zilizotengwa, hapa ikiwamo watoto, wa kiume na wa kike.

Kwa ujumla, mjadala huu unaonesha kuwa fasihi ya watoto ni daraja kati ya vizazi na ni darasa hai la historia, uraia, uzalendo na ujenzi wa taifa. Inawafanya watoto wawe wahusika hai katika simulizi za kumbukumbu za pamoja na kuwapa nafasi ya kuunda maana mpya kuhusu utumwa, ukoloni na taifa la Tanzania.

## 7.0 Hitimisho

Makala hii imeonesha kwa uwazi kwamba watoto wana nafasi kubwa katika historia ya mapambano dhidi ya utumwa na ukoloni, nafasi ambayo mara nyingi imepuuzwa

katika simulizi rasmi za kihistoria. Kupitia uchambuzi wa matini za Lihamba na Mulokozi pamoja na mitazamo ya watoto wasomaji, imebainika kuwa fasihi ya watoto si tu nyenzo ya kuburudisha, bali ni chombo cha kujenga uelewa wa kihistoria, kuimarisha maadili ya uraia, na kukuza utambulisho wa kitaifa. Watoto wanapojiweka katika nafasi ya wahusika wa fasihi, wanajiunda upya kama warithi wa mapambano, walinzi wa umoja na wabunifu wa taifa.

Kwa kutumia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, imeonekana kuwa watoto hawasomi tu historia, bali wanaifasili upya kwa kuhusisha simulizi na hali halisi za maisha yao ya sasa. Vivyo hivyo, kwa kutumia Nadharia ya Jumuiya Zilizobuniwa, matini hizi zinawasaidia watoto kuliona taifa kama urithi wa pamoja unaohitaji kulindwa na kila kizazi. Ushahidi wa kihistoria uliohusishwa katika makala unaimarisha hoja kuwa simulizi za watoto zinachangia utunzaji na uendelezaji wa kumbukumbu ya kihistoria ya Tanzania.

Kwa msingi huo, fasihi ya watoto inapaswa kupewa nafasi katika ufundishaji na ujifunzaji wa historia kwa sababu inawajenga watoto si kama watazamaji wa historia bali kama watengenezaji wa historia. Hivyo, makala hii inachangia kurejesha sauti ya mtoto katika mjadala wa kitaifa kuhusu kumbukumbu, urithi na ujenzi wa taifa, sauti ambayo ni muhimu kwa Tanzania ya sasa na ya baadaye.

## Marejeleo


Alpers, E. A. (1983). The Story of Swema: Female Vulnerability in Nineteenth-Century East Africa. Katika C.C. Robertson na M.A. Klein (Wah.), *Women and Slavery in Africa*. Madison: University of Wisconsin Press. Kur. 185-206.

Anderson, B. (1983). *Imagined Communities: Reflections on the Origin and Spread of Nationalism.* London: Verso.

Bakize, L.H., Ngugi, P.M.Y. na Lyimo, E.B. (2017). “Maendeleo ya Fasihi ya Watoto Nchini Tanzania na Kenya: Mkabala Linganishi.” *Kiswahili.* 80: Kur. 115-136.

Fish, S. (1980). *Is There a Text in This Class? The Authority of Interpretive Communities.* Cambridge: MA: Harvard University Press.

Geiger, S. (1987). “Women in Nationalist Struggle: TANU Activists in Dar es Salaam.” *The International Journal of African Historical Studies*. 20(1): Kur. 1–26.

Geiger, S. (1996). “Tanganyikan Nationalism as “Women’s Work”: Life Histories, Collective Biography, and Changing Historiography.” *The Journal of African History.* 37(3): Kur. 465–478.

Geiger, S. (1997). *TANU Women: Gender and Culture in the Making of Tanganyikan Nationalism, 1955–1965.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Guha, R. (1988). "On Some Aspects of the Historiography of Colonial India." Katika R. Guha na G.C. Spivak (Wah.), *Selected Subaltern Studies.* Delhi: Oxford University Press. Kur. 37-44.

Gwassa, G.C.K. (1969). "The German Interventions and the African Resistance in Tanzania." Katika I.N. Kimambo na A.J. Temu (Wah.), *A History of Tanzania.* Nairobi: East African Publishing House. Kur. 85-122.

Kollman, P. (2005). *The Evangelization of Slaves and Catholic Origins in Eastern Africa*. Maryknoll, NY: Orbis Books.

Lihamba, A. (1990). *Wimbo wa Sokomoko.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Lyimo, E.B. (2014). Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania. *Mulika*. 33: Kur. 33-45.

Magumba, J.M. (2025). African Abolitionists, Slave Narratives and Tourism in Bagamoyo. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mahenge, E.G. (2020). "Uchambuzi wa Dhima ya Msimulizi katika Bunilizi ya Watoto ya *Zindera*." *Kioo cha Lugha.* 18: Kur. 158-174.

Mosha, E. (2017). Uimarishaji wa Ujinsuke katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Hadithi Teule za Kiswahili za Watoto. *Kioo cha Lugha.* 15: Kur. 158-174.

Msacky, H. (2024). African Abolitionism and The Heritage of Slavery in Bagamoyo, 1960-2023. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1990). *Ngoma ya Mianzi*. Morogoro: ECOL Publications.

Mulokozi, M.M. (1991). *Ngome ya Mianzi.* Dar es Salaam: MPB Enterprises.

Mulokozi, M.M. (1996). *Moto wa Mianzi.* Morogoro: ECOL Publishers.

Ngugi, P.M.Y. (2014). Fasihi ya Watoto katika Kutekeleza Mahitaji ya Mtoto. *Kiswahili.* 77: Kur. 170-180.

Ngugi, P.M.Y. (2016). Usawiri wa Masuala Ibuka katika Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Kenya. *Mulika*. 35: Kur. 76-86.

Njogu, K. na R.M. Wafula. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jommo Kenyatta Foundation.

Nyachoga, S. na Liebst, M. (2024). "Rethinking Liberated Africans as Abolitionists: "Bombay Africans," Resistance, and Ritual Integration in Coastal Kenya, 1846–1900." *Slaveries & Post-Slaveries Journal. 7*(1). Inapatikana katika https://journals.openedition.org/slaveries/10820.

Omari, C.K. (1995). "Management of Tribal and Religious Diversity." Katika Legum, C. na Mmari, G. (Wah.), *Mwalimu: The Influence of Nyerere*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota. Kur. 23-31.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Rosenblatt, L.M. (1978). *The Reader, The Text, the Poem: The Transactional Theory of the Literary Work*. Carbondale, IL: Southern Illinois University Press.

Solomon, E. (2024). African Abolitionists and Memories of Slavery in Post-Abolition Ujiji, 1922-2023. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Spivak, G.C. (1988). Can the Subaltern Speak? katika C. Nelson na L. Grossberg (Wah.), *Marxism and the Interpretation of Culture.* University of Illinois Press. Kur. 271-313.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2006). *Muhtasari wa Somo la Uraia kwa Shule za Msingi Darasa la III-VII 2006*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2006). *Muhtasari wa Somo la Historia kwa Shule za Msingi Darasa la III-VII 2006*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.